

Title	Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili
Author(s)	Isack, Zainabu Kassu
Citation	外国語教育のフロンティア. 2019, 2, p. 259-269
Version Type	VoR
URL	<a href="https://doi.org/10.18910/71897">https://doi.org/10.18910/71897</a>
rights	
Note	

*Osaka University Knowledge Archive : OUKA*

<https://ir.library.osaka-u.ac.jp/>

Osaka University

# Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili

The Concept and Role of Family and Kinship in Swahili Culture

ISACK, Zainabu Kassu

## Abstract

The aim of this brief article is to highlight one aspect of Swahili Culture, that is the aspect of Family and Kinship relations under the title: *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili* (The Concept and Role of Family and Kinship in Swahili Culture). We define Culture as the sum total of social behaviours, traditions, customs and a total way of life of a particular society. Culture looks at the regular practices of the given society such as; when or what they eat, their dress codes, greetings, their etiquettes, taboos, their beliefs and so on (Isack 2018:105). This article is the continued efforts of the writer in enriching the knowledge on Swahili Culture and African Culture at large. As we mentioned in the previous article: *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili* (The Upbringing and Life Stages in Swahili Culture) (Isack 2018:105), there are challenges in the instruction of Swahili Language and its Culture to foreign learners due to the lack of enough reference materials designed for them. Thus, both instructors and learners of Swahili as a foreign language can utilize this work to narrow the current knowledge gap.

Keywords: Family, Kinship, Swahili culture

## Ikisiri

Lengo la makala hii fupi ni kuangazia kipengele kimojawapo cha utamaduni wa Kiswahili kipengele cha Familia na mahusiano ya nasaba chini ya mada: *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili*. Tunaufasili utamaduni kama ni jumla ya tabia, mila, desturi na mitindo ya maisha ya watu wa jamii fulani. Utamaduni unaangalia namna watu wanavyofanya mambo yao kwa kawaida kama vile; wakati gani au nini wanakula, mavazi yao, wanasalimiana vipi, mambo ambayo ni adabu, miiko yao, mambo wanayoamini n.k (Isack 2018:105). Makala hii ni mwendelezo wa juhudi za mwandishi katika kutajirisha maarifa juu Utamaduni wa Kiswahili na Utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla. Kama tulivyosema katika makala iliyopita: *Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2018:105), kuna changamoto katika ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili na Utamaduni wake kwa wanafunzi wageni kutokana na uhaba

wa rejea zinazowalenga wajifunzaji wageni. Hivyo basi, makala hii inapendekezwa kutumika kama rejea kwa wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ili kupunguza mwanya wa maarifa uliopo hivi sasa.

Keywords: Familia, Unasaba, Utamaduni wa Kiswahili

## 1. Utangulizi

Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (5); Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaolezea mpangilio wa makala hii. Sehemu mbili za mwanzo (yaani sehemu ya 2 na ya 3) zinatutambulisha zaidi kuhusiana na dhana ya familia na unasaba katika utamaduni wa Kiswahili. Sehemu ya pili (2) inataja majina ya familia, udugu au unasaba yanayotumika katika utamaduni wa Kiswahili na fasili zake. Sehemu ya tatu (3) inagusia mambo kadhaa ya kitamaduni yanayohusiana na familia na mahusiano ya nasaba kwa ujumla. Katika sehemu ya nne (4) tunazungumzia dhima ya familia na unasaba katika utamaduni wa Kiswahili, vilevile tunatalii baadhi ya methali za Kiswahili zinazohusiana na mambo ya familia au unasaba kwani tunaamini kuwa methali kama ilivyo kwa tanzu nyingine za kifasihi zinaakisi fikra na uhalisi wa mazingira ya maisha ya watu wa jamii husika. Na kuwa fasihi katika anavyobainisha Mulokozi (1996:15) ina dhima kadhaa za kitamaduni ikiwemo kuhifadhi na kurithisha amali za jamii. Dhima nyingine ni pamoja na kuburudisha, kukuza kudumisha na kuendeleza lugha, kuelimisha, kuasa na kurekebisha jamii. Hivyo basi, kwa kubainisha na kuzifafanua methali tajwa, tunaweza kujenga taswira halisi kuhusiana na mambo yahasuyo familia na unasaba katika utamaduni wa Kiswahili. Sehemu ya tano (5) na ya mwisho ni hitimisho; katika sehemu hii tunatoa muhtasari wa makala hii na mapendekezo kwa makala zijazo.

## 2. Majina ya nasaba au familia

Majina muhimu yanayotaja nasaba au uhusiano wa kifamilia katika Kiswahili ni pamoja na; Baba, mama, babu, bibi, kaka, dada, shangazi, mjomba, mama mdogo, mama mkubwa, ami, baba mdogo, baba mkubwa, binamu, mpwa, mzazi, binti, mjukuu, kitukuu, kilembwe.

### 2.1 Fasili ya majina ya nasaba/udugu/familia

Katika sehemu hii tunatoa fasili sahili ya mjina ya nasaba au uhusiano wa kifamilia kwa kuzingatia utamaduni wa Kiswahili.

Tukianza na *Baba*: huyu ni mzazi wa kiume. *Mama* ni mzazi wa kike. Babu ni mzazi wa kiume wa baba au mama yako: Ikiwa ni wa upande wa baba aghalabu huitwa *babu mzaa baba*, au *babu mzaa mama* ikiwa yeye ni wa upande wa mama yako. *Kaka* ni ndugu wa kiume. *Dada* ni ndugu wa

kike. *Shangazi* ni ndugu wa kike (dada) wa baba. *Mjomba* ni ndugu wa kiume (kaka) wa mama. *Mama mdogo* na *mama mkubwa* ni ndugu wa kike (dada) wa mama. *Ami*, *baba mdogo* au *baba mkubwa* ni ndugu wa kiume (kaka) wa baba. *Binamu* ni mtoto (wa kike au wa kiume) wa mjomba au shangazi. *Mpwa* ni mtoto wa ndugu wa kike (dada) au ndugu wa kiume (kaka). *Mzazi* ni baba au mama. *Binti* ni mtoto wa kike. *Mjukuu* ni mtoto wa mtoto wako (uzao wa tatu kutoka kwa wazazi wa mwanzo). *Kitukuu* ni mtoto wa mjukuu wako (yaani uzao wa nne kutoka kwa wazazi wa mwanzo). Na *kilembwe* ni mtoto wa kitukuu (uzao wa tano kutoka kwa wazazi wa mwanzo).

### 3. Mambo ya kitamaduni kuhusiana na familia au unasaba

Hapa tunazungumzia mambo anwai kuhusiana na dhana au fikra ya familia au mahusiano ya kinasaba kulingana na utamaduni wa Kiswahili.

#### 3.1 Kuhusu majina ya nasaba au uhusiano wa kifamilia.

Awali, katika utamaduni wa Kiswahili, majina ya *Shangazi*, *mama mkubwa*, na *mama mdogo* yana dhana tofauti kidogo yakilinganishwa na tamaduni nyingine. Kwa mfano katika Kiingereza majina yote yanatafsirika kwa jina moja, “aunt”. Kiswahili kwa upande mwingine, kinapambanua mahusiano hayo kwa dhana tofauti kulingana na unyeti wa utofauti wa mahusiano hayo katika utamaduni wa Kiswahili. Tukiangalia dhana ya jina *shangazi*, hili ni jina linaloeleza nasaba ya upande wa baba tu katika utamaduni wa Kiswahili. Kwa upande wa mama jina hilo halitumiki; dada wa mama yako si *shangazi* yako bali huitwa *mama mdogo* ikiwa yeye ni mdogo kuliko mama yako au *mama mkubwa* ikiwa yeye ni mkubwa kuliko mama yako.

Pili ni kuhusiana na majina *mjomba*, *ami*, *baba mkubwa* na *baba mdogo*. Majina haya yanaakisi tofauti nyeti za kidhana kuhusiana na nasaba kitamaduni. *Mjomba* ni jina linalotumika kwa nasaba ya upande wa mama tu katika utamaduni wa Kiswahili. Kaka wa baba yako si *mjomba* wako bali huitwa *ami* yako au *baba mkubwa* ikiwa yeye ni mkubwa kiumri kuliko baba yako au *baba mdogo* ikiwa yeye ni mdogo kiumri kuliko baba yako.

#### 3.2 Nani anahesabiwa kama Mwanafamilia?

Katika utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla, watu huhesabiwa kama sehemu ya familia kwa kuzingatia uhusiano wa damu yaani watu wenye nasaba moja. Uhusiano wa damu huchukuliwa kama uhusiano wenye nguvu na wa karibu sana katika tamaduni nyingi za Kiafrika. Sawa sawa na tamaduni nyingine nyingi duniani, wazazi na watoto ni sehemu ya familia ya karibu. Lakini katika utamaduni wa Kiswahili na tamaduni nyingi za Kiafrika, watu kama bibi, babu, wajukuu, wajomba, ami, shangazi, binamu, wapwa pia huchukuliwa kama ni nasaba ya karibu kwani

wanahesabiwa kama ni ndugu wa damu. Aidha, kuna dhana ya uhusiano wa kifamilia unaopatikana kwa kuoleana. Mtu anapooa au kuolewa katika familia fulani, ni kawaida katika utamaduni wa Kiswahili kusikia fikra kama familia hizo zimeungana na kuwa familia moja. Wazazi wa mke au mume yani wakwe kwa mfano, wanaheshimiwa na kupewa nafasi ya kipekee katika tamaduni za Kiafrika. Zaidi, tofauti na baadhi ya tamaduni, wanyama na viumbe wengine katu hawahesabiwi kama sehemu ya familia. Mathalan, ni jambo la kustusha kitamaduni (Cultural shock) kwa mswahili unaposikia mtu akitambulisha familia yake na kuhesabia wanyama wafugwao nyumbani (pets) kama mbwa na paka kama sehemu ya familia yake.

### 3.3 Ukubwa wa familia

Familia na koo za Kiafrika kwa jumla ni familia kubwa na pana sana. Si tu zinahusisha familia ya karibu yaani wazazi na watoto wao, bali pia ndugu wanaohusiana kwa damu (wenye nasaba moja), na watu wanaonasibiana kwa kuoleana. Kama tulivyotangulia kusema awali (3.2), watu wanapooana, inahesabiwa kama koo mbili au familia mbili zimeungana na hivyo kuongeza ukubwa au upana wa familia. Kupata watoto katika ndoa hupewa umuhimu wa kipekee katika jamii za Kiafrika kwani jambo hili huchukuliwa kama ndiyo njia sahihi ya kuendeleza kizazi na kukuza jina la familia kwani hujenga uhusiano wa damu. Aghalabu kinasaba watoto huhesabiwa upande wa baba na hivyo kuchukua ubini wa baba katika jamii ya waswahili ambayo ni jamii ya mfumo wa kuumeni (patrilineal society).

### 3.4 Majukumu ya Kifamilia

Katika sehemu hii tunafafanua majukumu ya kifamilia kwa kuyagawa katika makundi matano yafuatayo; wanaume, wanawake, wazazi, watoto, ndugu na jamaa wengine.

#### 3.4.1 Wanaume

Katika utamaduni wa Kiswahili na tamaduni nyingi za Kiafrika, watoto wa kiume au wanaume hupewa kipaumbele zaidi katika mambo mengi ya familia hasa kwa kuzingatia majukumu yao. Katika mirathi kwa mfano, kwa sharia za Kiislamu fungu la mwanamume mmoja ni sawa na fungu la wanawake wawili; wanaume hupewa sehemu kubwa ya urithi kuliko wanawake kwani wanahesabiwa kama ndio watu wanaoendeleza familia au nasaba na watu wenye jukumu la kuwatunza (kwa mali/fedha) watoto wa kike/wanawake/ wake/dada zao.

Babu, baba, mume, kaka au mtoto wa kiume ndio wenye mamlaka zaidi na viongozi katika familia; Mwanamume ndiye kichwa cha familia. Wanaume wana nafasi zaidi katika kushauri na kuamua mambo ya familia. Mwanamke yupo chini kimamlaka; mathalan mke yupo chini ya uangalizi

wa mume, mtoto wa kike yupo chini ya mamlaka ya mzazi, na hata dada yupo chini kimamlaka akilinganishwa na nduguye wa kiume. Pia, ni wajibu wa mwanamume au mume kutafuta kipato ili kutunza familia.

#### **3.4.2 Wanawake**

Kazi ya wanawake kitamaduni ni kutunza nyumba na watoto. Kazi hizo ni pamoja na kupika, usafi wa nyumba, kufua na kuwalea watoto katika maadili yanayokubalika. Kwa muda mrefu katika jamii za Kiafrika kumekuwa na mfumo na dhana ya kitamaduni kwamba nafasi ya mwanamke au mtoto wa kike ni nyumbani au jikoni. Utamaduni huo hata hivyo unabadilika pole pole katika zama hizi. Wasichana wengi zaidi wanasoma aghalabu mpaka kufikia elimu ya juu, na wanawake wanafanya kazi za ofisini au bishara na kushika nafasi kadhaa muhimu katika jamii japokuwa bado hakuna uwiano ikilinganishwa na wavulana au wanaume.

#### **3.4.3 Wazazi**

Kwanza kabisa, jukumu la wazazi ni kuwatunza watoto kwa hali na mali katika mahitaji yao ya msingi kama kuwapa chakula, malazi, mavazi, kutunza afya zao, kuhakikisha watoto wanapata elimu n.k. Wazazi pia wana jukumu la kuwalea na kuwafunza adabu au maadili watoto wao na hata kuwaadhibu pale wanapokosea. Mtoto asiye na maadili huchukuliwa kama zao la kukosa kufunzwa au mtoto aliyeshindikana kufunzika na wazazi wake. Zaidi, katika jamii za Kiafrika na hasa zamani wazazi walikuwa ni washauri na waamuzi wakuu katika mambo yote yanayomhusu mtoto; kwa mfano mambo ya elimu ya mtoto, mahusiano ya ndoa n.k.

#### **3.4.4 Watoto**

Watoto wanawajibika kuwaheshimu wazazi na ndugu wengine, kusaidia shughuli za nyumbani, kuwa na uhusiano mzuri na ndugu wengine na kuwatunza wazazi wao pindi wanapokuwa wazee.

#### **3.4.5 Ndugu na jamaa**

Ndugu na jamaa wengine wana wajibu wa kushirikiana na kusaidiana kwa hali na mali katika mambo ya furaha au matatizo. Na kutofanya hivyo ni sawa sawa na kuvunja udugu au kuharibu uhusiano katika familia au koo.

### **3.5 Adabu na Miiko**

Kitamaduni kila jamii ina seti ya mambo yanayofikiriwa kuwa ni mazuri yaani *adabu* kwa upande mmoja na seti ya mambo ambayo si vizuri kabisa kufanya; *miiko* kwa upande mwingine.

Hapa tutaja baadhi tu ya mambo ya adabu na miiko yanayoendana na mahusiano ya familia au nasaba katika utamaduni wa Kiswahili. Kwanza, ni muhimu sana na ni adabu kuwaheshimu wakubwa na hasa wazazi. Pili, ni vizuri kuwa mkarimu na kuwasaidia wanafamilia, ndugu na jamaa zako kwa hali au kwa mali. Tatu, ni mwiko watu wenye udugu wa damu/nasaba moja au mahusiano kadhaa ambayo yanahesabiwa kama ni ya mwiko kuoana. Mathalani kwa mujibu wa imani ya Kiislamu kurani inataja kuwa imeharamishwa kwa watu kuwaoa mama zao, binti zao, dada zao, shangazi zao, binti wa ndugu wa kiume, binti wa dada, mama aliyekunyonyesha, dada kwa kunyonya, mama wa mkeo, watoto wa kambo walio katika ulinzi wako waliozaliwa na mke uliyemuungilia, wake wa watoto wako, na kuwaoa dada wawili (kwa wakati mmoja). Nne, ni jambo la mwiko kwa mtoto wa kiume kuutazama mwili wa mzazi wa kike, au mke au mume kuona mwili wa mkwe wake (wa jinsia tofauti na yeye; yaani mke kwa baba mkwe, na mume kwa mama mkwe). Na ni laana ikiwa mzazi wa kike atamuonyesha mtoto wa kiume mwili wake na kusema maneno ya kumlaani. Watu wanaamini mtoto huyo atapatwa na laana hiyo na atakuwa na maisha mabaya. Imani hii imejengeka sana katika tamaduni kadhaa za Kiafrika.

#### **4. Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili**

Sehemu hii inazungumzia dhima ya familia na mahusiano ya nasaba na kutalii baadhi ya methali za Kiswahili zinazohusiana na mada husika.

##### **4.1 Umuhimu wa familia na nasaba**

Katika jamii za Kiafrika ikiwemo jamii ya Kiswahili kama zilivyo jamii nyingi duniani, familia au koo ni taasisi muhimu kabisa katika maisha ya binadamu. Ndio namna ya kuendeleza nasaba, pia ni taasisi ya kuwafunza na kuwarithisha watoto amali za jamii (kabla na hata baada ya mtoto kwenda shuleni). Kama ilivyobainishwa juu (sehemu ya 3.4) kuhusu majukumu ya kifamilia ni dhahiri kuwa wajibu mkubwa unawaangukia wazazi na watoto; wazazi wana wajibu nyeti katika kuwatunza, kuwalinda, kuwaongoza na kuhakikisha maisha mazuri kwa watoto walau mpaka wanapofika umri wa kujitegemea. Watoto pia wana wajibu mkubwa wa kuwaheshimu wazazi wao. Watoto pia wanatarajiwa si tu kuwaheshimu wazazi bali pia, kuwatunza wazazi wao wanapokuwa wazee. Ndugu wengine kwa upande mwingine wanatarajiwa kushirikiana na kusaidiana katika mambo mbalimbali; kwa mfano katika sherehe, misiba, wakati wa matatizo mengine pia kama ugonjwa, kukosa pesa, maafa n.k.

##### **4.2 Methali za Kiswahili kuhusiana na familia na mahusiano ya nasaba**

Methali ni usemi mfupi wa kimapokeo unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito

yaliyotokana na tajriba (uzoefu wa maisha) ya jamii inayohusika (Mulokozi 1996: 36). Methali kwa kawaida hubeba maana pana kuliko maneno yanayotumiwa ndani ya methali yenyewe. Methali za Kiswahili kama zilivyo katika lugha nyingine hurejelea sana maisha na mazingira watu waishimo. Methali hutumika kwa kuonya, kufunza, kufariji, kueleza fikra au falsafa ya jamii husika juu ya mambo mbali mbali n.k. Kuna methali kadhaa katika Kiswahili zinazohusu kwa namna moja au nyingine mambo ya familia na mahusiano ya nasaba. Basi, ni fursa nzuri tukizitalii baadhi ya methali hizo kwa kufafanua maana na matumizi ya methali hizo. Ufafanuzi huo, unatarajiwa kutusaidia kufahamu kiundani fikra za Waswahili juu ya dhana na dhima ya mambo yahasuyo familia na uhusiano wa kinasaba katika utamaduni wa Kiswahili. Kwa kila methali; tutataja methali yenyewe sambamba na tafsiri ya methali hiyo/au methali kama hiyo kwa Kiingereza (katika mabano), ikifuatiwa na maana yake na mwisho tutadokeza muktadha wa matumizi ya methali husika.

**i. Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu** (*He who is not taught by his own mother, is taught by the world*). *Maana*; Kwa mtoto ambaye anafunzwa na wazazi lakini hawasilizi, waswahili wanaamini mtoto huyo atafundishwa na dunia yaani kutokana na tajriba yake ya maisha aghalabu kupitia matatizo au matokeo mabaya ya vitendo vyake. *Matumizi*; Methali hii inatufunza umuhimu wa kufuata mafunzo na ushauri wa wazazi.

**ii. Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu** (*He who does not listen to the leader/elders, breaks a leg (fails)*). *Maana*; Mtu asiyesikiliza au asiyefuata ushauri wa wakubwa, atapatwa na mambo mabaya au matokeo mabaya. Wakubwa ni watu wanaokuzidi umri au cheo na inaaminika wana tajriba zaidi au busara zaidi ya walio chini yao. *Matumizi*; Ni muhimu kusikiliza au kufuata ushauri wa wakubwa.

**iii. Damu nzito kuliko maji** (*Blood is thicker than water*). *Maana*; Uhusiano wa watu ambao ni ndugu aghalabu uhusiano wa damu ni wenye nguvu na uhusiano muhimu zaidi kuliko uhusiano mwingine wowote. *Matumizi*; Methali hii inatadokeza thamani na umuhimu wa uhusiano wa watu wenye nasaba moja.

**iv. Hakuna kama mama** (*There is no one like a mother*). *Maana*; Hakuna mtu muhimu katika maisha kushinda mama yako. Waswahili wanafikiri hakuna upendo unaozidi upendo wa mama. Mama yako atakutunza na kukujali katika hali yoyote. *Matumizi*; Methali hii hutumika kuwapa heshima na kutambua umuhimu wa akina mama.

**v. Kubeba mimba si kazi, kazi kulea mwana** (*It is not hard to nurse a pregnancy, but it is hard to*



*rear a child*). *Maana*; Tunajua kwa mwanamke kubeba mtoto tumboni wakati wa mimba kwa miezi tisa si kazi rahisi, lakini waswahili wanafikiri kazi ya kumlea mtoto baada ya kuzaliwa ndiyo ngumu zaidi. Pia, methali hii ina maana kuwa jukumu la mzazi si tu kumzaa mtoto, mzazi ana jukumu la kumlea mtoto wake. *Matumizi*; Methali hii inatukumbusha tusitarajie urahisi katika malezi ya watoto, hasa tunapokuwa na wakati mgumu katika malezi. Pia, methali hii inasisitiza umuhimu wa wazazi kuwalea watoto wao.

**vi. Mchelea mwana kulia hulia yeye** (*He, who fears the crying of a child, will cry himself/Spare the rod and spoil the child*). *Maana*; Anayeogopa kumwona mtoto wake akilia au anayehofia kumuadhibu au kumrudi mtoto wake anapokosea, basi baadaye atalizwa yeye au atahuzunishwa yeye kwa tabia mbaya au kukosa adabu kwa mtoto wake. *Matumizi*; Methali hii inawaonya wazazi juu ya umuhimu wa kuwafundisha watoto maadili au adabu hata ikibidi kumrudi pale anapokosa.

**vii. Mkono mmoja haulei mwana** (*One hand cannot raise a child/It takes the village to raise the child*). *Maana*; Mtu mmoja peke yake hawezi kumlea mtoto kikamilifu, anahitaji msaada wa watu wengine pia. *Matumizi*; Methali hii inatadokeza umuhimu wa jamii kushirikiana katika malezi ya watoto.

**viii. Mtegemea cha nduguye hufa masikini** (*One who always depends on his brother will die poor*). *Maana*; Mtu anayetegemea mali ya ndugu yake atakufa hali yu masikini. *Matumizi*; Methali hii inasisitiza umuhimu wa mtu kufanya kazi na kujitafutia kipato, siyo kuwategemea watu wengine aghalabu ndugu.

**ix. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha mamaye** (*A child follows its mother's footsteps*). *Maana*; Mama wa Kiswahili ambebapo mwanawe aghalabu humbeba kwa kumweleka mgongoni mwake. Kwa hivyo mtoto huyo anapobebwa, sehemu aionayo ya mwili wa mamake ni kisogo. *Matumizi*; Methali hii hutumiwa kuonyesha kwamba mtoto hufuata tabia ya mamake au mlezi wake.

**x. Mtoto akililia wembe mpe umkate** (*If a child cries for a razor give it to him for it to cut him /Let the child learn by experience*). *Maana*; Mtoto ambaye anakanywa lakini hasikilizi ushauri wa wakubwa, anaachwa ili ajifunze kutokana na tajriba yake aghalabu kupitia matokeo mabaya ya kitendo chake. *Matumizi*; Methali hii inatufunza umuhimu wa kufuata ushauri wa wakubwa pia.

**xi. Mtoto akinyea mkono haukatwi** (*When a child defecates on your palm it is not cut/ When a*

*Child makes a mistake s/he needs a second chance*). *Maana*; Mtoto au mdogo anapokosea anahitaji kusahihishwa na kusamehewa. *Matumizi*; Methali inatufunza umuhimu wa kusamehe mtu aghalabu aliye chini yako anapokukosea.

**xii. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo** (*The parents' upbringing will determine the character of a child*). *Maana*; Namna unavyomlea mtoto wako, ndivyo atakavyokuwa atapokuwa mtu mzima. Kama ulimlea vizuri kwa kumfundisha maadili basi atakua mtu mzuri. Kama hutamfunza maadili utotoni, basi atakuwa hana maadili pia atakapokuwa mtu mzima. *Matumizi*; Methali hii inatudokeza umuhimu wa kuwafundisha watoto maadili au adabu. Mzazi ambaye hakumlea mtoto wake vyema huweza kukosolewa kwa methali hii.

**xiii. Mtoto wa nyoka ni nyoka** (*The son of a snake is a snake/Like father like son*). *Maana*; Mtu huathiriwa na ubaya au uzuri wa tabia za wazazi wake. *Matumizi*; Mtu aliyechukua ubaya wa wazazi wake huweza kufunzwa kwa methali hii.

**xiv. Radhi ni Bora kuliko mali** (*Blessing is better than wealth*). *Maana*; Mtu anayewaheshimu wazazi wake na akapata baraka zao, waswahili wanaamini mtu huyo ataishi maisha mazuri, ya furaha na mafanikio. Na akiwatendea kinyume wazazi akakosa radhi zao kila alifanyalo haliwezi kumnyookea. *Matumizi*; Methali hii hutumika kuwafunza watu kuwaheshimu na kuwathamini wazazi wao.

**xv. Samaki mkunje angali mbichi** (*Bend the fish while it is still fresh/Hit the iron while it is hot*). *Maana*; Mfunze mtu adabu au maadili wakati wa utoto, akishakua mtu mzima ni vigumu kumfundisha. *Matumizi*; Methali hii ni funzo kwa wazazi kuwafundisha watoto maadili au adabu mapema.

**xvi. Sikio halipiti kichwa** (*The ear is not greater than the head*). *Maana*; Sikio daima lipo chini ya kichwa; mdogo daima hawezi kumzidi au kumpita mkubwa. *Matumizi*; Methali hii inalenga kuisisitiza umuhimu wa mdogo kumuheshimu mkubwa.

**xvii. Uchungu wa mwana aujua mzazi/mama** (*The parent feels the pain of a child/only the mother knows the labour of childbirth*). *Maana*; Mtu anayeyejua thamani ya kweli ya mtoto ni mzazi wake/mama yake. Wazazi wana upendo mkubwa kwa watoto wao na wanawajali sana. *Matumizi*; Methali hii inatukumbusha thamani au mapenzi ya mzazi kwa mtoto wake.

**xviii. Udugu si kufanana udugu ni kufaana** (*Your brother is the one who assists you not the one who looks like you*). *Maana*; Haitoshi kusema mtu ni ndugu yako kwa sababu mnanafanana sura, undugu wa kweli ni kwa kusaidiana. Pia, rafiki wa kweli au mtu ambaye anakusaidia ni sawa sawa na ndugu. *Matumizi*; Methali hii inatufunza umuhimu wa kusaidiana. Na kuwa mtu anayekusaidia ni sawa na nduguyo hata kama hamna uhusiano wa kweli wa damu.

Methali hizi zinazohusiana na mambo ya familia au unasaba zinaweza kutusaidia kubaini fikra za kitamaduni na falsafa ya waswahili hasa kuhusu masuala kama umuhimu wa wazazi/wakubwa na nafasi na wajibu wa wazazi katika malezi ya watoto. Kupitia methali tunajua kuwa wazazi wana wajibu mkuu katika maisha ya watoto kama vile kuwafunza watoto maadili, kuwarekebisha na hata kuwa mfano bora mbele ya watoto wao kama isemavyo methali “*Mtoto wa nyoka ni nyoka*”. Pia, zinatodokeza kuhusu umuhimu au uthabiti wa uhusiano wa damu na ndugu kusaidiana. Methali hizo hutumika kuonya, kufunza kuakisi mazingira ya maisha, kueleza falsafa ya waswahili kuhusu mada husika na hata kutolea mfano.

## 5. Hitimisho

Makala hii imeangazia kipengele kimojawapo cha Utamaduni wa Kiswahili yaani Familia na mahusiano ya kinasaba chini ya mada: *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili*. Kwanza tumejaribu kufafanua kwa lugha nyepesi dhana au majina yanayotaja mahusiano ya kifamilia au ya kinasaba. Pili, tumeainisha baadhi ya mambo ya kitamaduni yanayofungamana na majina au masuala yahusuyo familia au nasaba. Tatu, tumefafanua dhima ya familia na unasaba na kusema kuwa familia ndio taasisi yenye dhima muhimu katika maisha ya binadamu si tu kwa kuwa ndio namna ya kuendeleza nasaba bali pia kama njia ya kuwafunza watoto na kuwarithisha amali za jamii. Nne, tumetalii baadhi ya methali zinazohusiana na familia au mahusiano ya kinasaba kwa kufafanua maana na matumizi ya methali hizo tukiamini, kama ilivyo kwa tanzu nyingine za fasihi methali zinaakisi jamii. Hivyo basi, methali hizo zinaweza kutilia mkazo na kutupa taswira halisi zaidi juu ya fikra, na mafunzo mbali mbali kuhusu umuhimu na wajibu au dhima ya familia na unasaba katika utamaduni wa Kiswahili. Kwa mfano, kupitia methali tunafahamu kuwa wazazi wana wajibu mzito na nafasi ya pekee katika maisha na malezi ya watoto.

Ni matumaini ya mwandishi kuwa kazi hii itapunguza mwanya wa maarifa katika ufundishaji wa Kiswahili na Utamaduni wake hususan kwa wanafunzi wageni. Makala hii inapendekezwa kutumiwa na wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya Kigeni. Pia, mwandishi anapenda kutukumbusha kuwa mambo yanayoutambulisha utamaduni wa watu ni mengi na anwai, hivyo basi tuweke juhudi katika kuangazia vipengele zaidi kuhusiana na utamaduni wa Kiswahili na utamaduni

wa Kiafrika kwa ujumla. Baadhi ya vipengele vinavyopendekezwa kujadiliwa katika kazi zijazo ni kama vile; desturi za salamu, chakula, mavazi, dini, imani na falsafa ya maisha, mambo ya adabu na miiko, lugha, fasihi, sanaa na burudani n.k.

### **Marejeo**

Abudu, Maryam & Baruwa Abdala

1981 *Methali za Kiswahili. Maana na Matumizi (2)*, Shungwaya Publishers Ltd, Nairobi.

1981 *Methali za Kiswahili. Maana na Matumizi (3)*, Shungwaya Publishers Ltd, Nairobi.

Buchanan, Daniel Crump

1965 *Japanese Proverbs and Sayings*, University of Oklahoma Press, Norman, Oklahoma.

Isack, Zainabu Kassu

2018 “Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika *Frontier of Foreign Language Education 1*, 105-118.

Mulokozi, M. M

1996 *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Ukurasa 15, 36.

Ndalu, Ahmed & King’ei Kitula G.

1994 *Kamusi ya Methali za Kiswahili*, East African Educational Publishers Ltd, Nairobi.

Taasisi ya Taaaluma za Kiswahili (TATAKI)

2014 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la Tatu)*, Oxford University Press, Nairobi.